

# MONITORING LEARNERS PROGRESS

SASON  
002

GREDI YA 4, MWAKA: 2021

KISWAHILI: LUGHA

Muda: Saa 1 Dak. 40

## SEHEMU 1: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

Mwalimu amuulize mwanafunzi maswali yafuatayo.

1. Hujambo? \_\_\_\_\_  
(Mwanafunzi ajibu)
2. Taja chakula ukipendacho. \_\_\_\_\_  
(Mwanafunzi ajibu)
3. Unajua kukipika chakula hicho? \_\_\_\_\_  
(Mwanafunzi ajibu)
4. Chakula hicho hupatikana wapi? \_\_\_\_\_  
(Mwanafunzi ajibu)
5. Chumba cha kupikia chakula huitwaje? \_\_\_\_\_  
(Mwanafunzi ajibu)

### Vigezo vya Kutathminia - Kusikiliza na Kuzungumza

Kiwango cha utendaji	4	3	2	1
Upeo / Alama	5	4	3	0 - 2

## SEHEMU 2: KUSOMA KWA SAUTI

(Alama 5)

Mwanafunzi asome kifungu hiki kwa sauti.

Juma alialikwa katika sherehe ya kuadhimisha siku ya kuzaliwa kwa Ali. Aliamka asubuhi na mapema. Akaoga na akavaa nguo yake safi. Hakutaka kuchelewa hata kidogo. Viatu vyake pia vilikuwa safi ajabu. Alitembea polepole hadi kwa akina Ali.

Huko aliwapata watoto wengine. Kila mtu alikuwa mwenye furaha kuu. Hakika sherehe ilikuwa imeanza kunoga. Mamake Ali aliwaletea sharubati na biskuti. Walifurahia sana. Hatimaye keki ililetwa. Ali aliambiwa aikate huku watoto wenzake wakiimba. Kulikuwa na shangwe, vifijo na nderemo.

### Vigezo vya Kutathminia - Kusoma

Kiwango cha utendaji	4	3	2	1
Maneno yaliyosomwa katika dakika moja	60 na zaidi	41 - 60	21 - 40	0 - 20

**SEHEMU 3: UFAHAMU (Alama 5)**

Soma vifungu hivi kisha ujibu maswali.

**(a) REHEMA**

Rehema ni mwanafunzi katika shule ya msingi ya Bidii. Yuko katika gredi ya nne. Kila siku yeye huamka saa kumi na mbili. Huwa anajitayarisha kabla ya kupata kiamshakinywa. Huwa anapenda kunywa uji.

- i) Rehema huenda shule gani? \_\_\_\_\_
- ii) Rehema yuko katika gredi gani? \_\_\_\_\_
- iii) Rehema huamka saa ngapi? \_\_\_\_\_
- iv) Rehema hupenda kunywa nini? \_\_\_\_\_
- v) Hadithi hii ni kuhusu nani? \_\_\_\_\_

**(b) SUNGURA NA NDOVU**

Sungura na ndovu walikuwa marafiki hata ingawa sungura alikuwa mdogo naye ndovu mkubwa. Wote walipenda kula nyasi. Baada ya kula nyasi walienda kunywa maji katika mto Baraka. Huko walikuwa wakipatana na rafiki yao pundamilia.

- i) Nani alikuwa mkubwa? \_\_\_\_\_
- ii) Nani alikuwa mdogo? \_\_\_\_\_
- iii) Wote walipenda kula nini? \_\_\_\_\_
- iv) Walikuwa wakienda katika mto Baraka kufanya nini? \_\_\_\_\_
- v) Walikuwa wakipatana na nani mtoni? \_\_\_\_\_

**Vigezo vya Kutathminia - Ufahamu**

Kiwango cha utendaji	4	3	2	1
Upeo / Alama	10	7 - 9	4 - 6	0 - 3


**SEHEMU 4: SARUFI**

Kanusha sentensi.

- 1. Mtoto anakunywa maziwa. - \_\_\_\_\_
- 2. Mgeni aliwasili jana. - \_\_\_\_\_
- 3. Leta kile kiti hapa. - \_\_\_\_\_
- 4. Mama ameenda sokoni. - \_\_\_\_\_

Andika majina ya maumbo.


5.




6.



7.



8.



Andika kinyume cha maneno haya.

9. Mchana - \_\_\_\_\_  
10. Mwangaza - \_\_\_\_\_  
11. Cheka - \_\_\_\_\_  
12. Funika - \_\_\_\_\_

Andika sentensi kwa wingi.

13. Kiti hiki kimevunjika.  
\_\_\_\_\_  
14. Mwanafunzi amenunua kiatu.  
\_\_\_\_\_  
15. Nguo yangu ni safi.  
\_\_\_\_\_  
16. Mti huu ulikatwa.  
\_\_\_\_\_

Andika tarakimu kwa maneno.

17. 86 - \_\_\_\_\_  
18. 59 - \_\_\_\_\_  
19. 164 - \_\_\_\_\_  
20. 210 - \_\_\_\_\_

Vigezo vya Kutathminia - Sarufi

Kiwango cha utendaji	4	3	2	1
Upeo / Alama	19 - 20	17 - 18	7 - 12	0 - 6

**SEHEMU 4: KUANDIKA**

**INSHA**

Andika insha juu ya:

**DARASA LETU**

A series of approximately 25 horizontal lines provided for writing an essay.

**Vigezo vya Kutathminia - Kuandika**

Kiwango cha utendaji	4	3	2	1
Upeo / Alama	10	7 - 9	4 - 6	0 - 3